MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA


**Na: 26. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Juni 1-10, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Juni 11-20,2019**

**Muhtasari**

- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia uvunaji,ukaushaji na utunzaji wa mazao .
- Maeneo mengi ya nchi yamepata vipindi vya hali ya ukavu kwa kipindi cha mwezi june 1-10,2019.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua kuendelea kuwepo kaskazini mwa dunia na kuwepo katika nchi yetu hususan maeneo ya ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi liliendelea, hali hii ilisababisha kufanyika kwa migandamizo midogo ya hewa pamoja upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka kusini mashariki na kuelekea pwani ya kaskazini mwa Tanzania, hivyo kusababisha unyevu zaidi kuelekea maeneo ya pwani ya kaskazini. Joto la bahari la chini ya wastani lilikuwa katika eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo iliwezesha kuimarika kwa mifumo ya mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususan katika ukanda wa ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Juni 1- 10, 2019

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2019

Kwa kipindi hicho maeneo mengi ya nchi yalikua makavu isipokua maeneo maeneo machache ya ukanda wa ziwa Viktoria na nyanda za juu kaskazini magharibi hususan mkoa wa mara na wilaya ya Ngorongoro ambayo yamepata mvua za nje ya msimu. Kiasi cha mvua kilichopimwa ni kati ya 26mm na 100mm kama inavyojionesha kenye kielelezo.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2019

Katika kipindi hicho cha dekadi, baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka wakulima walikuwa wanajihusisha zaidi na uvunaji wa mahindi na maharage, isipokua kwa maeneo ya mikoa ya Mbeya na Njombe ambako zao la mahindi lilikua katika hatua ya kukomaa. Ngano imeripotiwa kuwa katika hali nzuri kwenye hatua ya kuchanua kwa mkoa wa Mbeya. Maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan mkoa wa Kagera shughuli za uvunaji wa maharage zimeanza. Kwa upande mwingine uvunaji wa mpunga uliendelea katika mikoa ya Tabora, Mwanza, Rukwa,Tanga,Pwani na Manyara. Wakulima mkoani Kigoma, Mwanza, na Shinyanga wanaendelea na uvunaji wa pamba.Kwa kipindi hicho maeneo mengi ya nchi yamepata upungufu wa unyevunyevu wa udongo. Maji na malisho ya mifugo nchini kwa ujumla viliendelea kuwa katika hali nzuri

isipokuwa kwa mkoa wa Dodoma ambako kumejitokeza upungufu kiasi.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mitiririko wa maji kwenye mito vimeendelea kupungua kutoka na kuisha kwa msimu wa mvua .

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda wa kuendelea kuwepo maeneo ya Ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuendelea, na inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka kusini mashariki na kuelekea pwani ya kaskazini mwa Tanzania. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo inamchango mdogo katika kusababisha mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususan katika ukanda wa Ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi. Upepo unatarajiwa kuvuma kutoka mashariki kwa pwani yote na maeneo ya karibu kwa wiki ya kwanza ya dekadi na kuvuma kutoka magharibi kwa wiki ya pili ya dekadi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2019

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Maeneo ya Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba yanatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

Maeneo ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa makavu na mawingu kiasi .

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20,2019

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi itasaidia shughuli za uvunaji, ukaushaji na uhifadhi wa mazao. Ingawaje hali hii ya ukavu itapelekea upungufu wa maji na malisho ya mifugo. Wafugaji wanashauriwa kutumia vizuri rasilimali za marisho na maji na kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2019.

.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo huwa yanakabiliwa na upungufu wa maji.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***